


jarida la

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO


Jarida la Mtandaoni

www.michezo.go.tz

Julai 03, 2022



Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo



TAHARIRI

TAMASHA LA UTAMADUNI LAIFUNGUA TANZANIA



Mhariri
JOHN MAPEPELE

Tamasha kubwa la Kitaifa la Utamaduni limezinduliwa jana na Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa, ambapo shughuli mbalimbali za utamaduni zimefanyika ikiwemo ngoma na maonesho ya vyakula na historia mbalimbali za makabila ya Tanzania.

Tamasha hilo la kwanza lililoandaliwa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, limefanyika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na kukutanisha mikoa 24 kati ya 26 ambapo ni mkoa wa Shinyanga na Geita hawakushiriki.

Kufanyika kwa Tamasha hilo ni maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa mkoani Mwanza mwezi Septemba mwaka jana wakati wa kuvikwa uchifu Hangaya.

Kimsingi tamasha hili limejumuisha vitu vikubwa vitatu, shughuli za utamaduni ambazo ni maonesho ya ngoma na vyakula vya asili, matembezi ya kiutamaduni, usiku wa taarabu na maadhimisho ya siku ya Kiswahili.

Vitu hivyo vyote vitatu vikubwa kwa pamoja ni ubunifu ambao umefanya wananchi kufurahia kuona tamaduni zao kwa wakati mmoja katika matukio ya kijamii.

Matukio haya yamefungua historia mpya ya nchi yetu ya kuyatumia ili kutangaza nchi yetu.

Tunapongeza jitihada hizi zinazofanywa na Serikali tunaamini huu ni mwanzo mzuri wa kutumia utamaduni katika kuitangaza nchi yetu.

Kazi iendelee.

BODI YA WAHARIRI

Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

Dkt. Hassan Abbasi

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

Saidi Yakubu

Mhariri

John Mapepele

Waandishi

**Eleuteri Mangi
Shamimu Nyaki
Eliphace Marwa**

Wapiga Picha

Joseph Kigingi

Projestus Binamungu

Abubakar W Kafumba

Msanifu

Abubakar W Kafumba



Mhe. Majaliwa Azindua Tamasha, Ashangazwa na Teknolojia ya Nyuki Kupinga Ukoloni

Na Mwandishi wetu

Tamasha kubwa la Kitaifa la Utamaduni limezinduliwa leo na Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa, ambapo shughuli mbalimbali za utamaduni zimefanyika ikiwemo ngoma na maonesho ya vyakula na historia mbalimbali za makabila.

Tamasha hilo la kwanza lililoandaliwa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, limefanyika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na kukutanisha

mikoa 24 kati ya 26 ambapo ni mkoa wa Shinyanga na Geita tu hawakushiriki.

Tamasha hilo ni maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa Mwanza Septemba mwaka jana wakati wa Kuvikwa uchifu Hangaya.

Moja ya mabanda ambako Waziri Mkuu alionesha kufutiwa nalo ni Banda la Mkoa wa Singida ambapo alielezwa jinsi teknolojia ya kutumia nyuki

ilivyotumika kupambana na ukoloni.

Mmoja wa machifu wa kale wa Wanyaturu, Malkia Liti, inaelezwa alikuwa na uwezo wa kuwaamrisha nyuki kuwashambulia askari wa kikoloni na kuulinda himaya yake kwa muda mrefu hadi alipokuja kusalitiwa baadaye.

Kwa heshima yake uwanja wa michezo mkoani Singida kwa sasa umetoka kuitwa Namfua hadi kuwa Uwanja wa Liti.



Waziri Mkuu Azindua Kitabu cha Muongozo wa Maadili ya Mtanzania

Na Eliphace Marwa, Dar es Salaam

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) amezindua rasmi kitabu cha Muongozo wa Maadili ya Mtanzania Julai 2, 2022 jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na washiriki wa Tamasha la Kwanza la Kitaifa la Utamaduni, Waziri Mkuu amesema kuwa maadili ya

Mtanzania yamekuwa yaki-poromoka siku hadi siku, hivyo kitabu hicho kitumike katika kurudisha madili kwa vijana wa Kitanzania.

“Vijana wa Kitanzania wamekuwa na maadili mabaya kutokana na Maendeleo ya teknolojia hivyo niwaombe viongezi wa kimila mtusaidie katika hili kwani tamasha hili linaonesha

asili ya mtanzania kuanzia mavazi hadi chakula,” alisema Waziri Mkuu Majaliwa.

Waziri Mkuu pia amezindua Tamasha la Kwanza la Kitaifa la Utamaduni ambalo limeshirikisha washiriki toka mikoa 24 ya Tanzania bara na Machifu 50.



Waziri Mkuu Mhe. Majaliwa Apongeza Kufanyika kwa Tamasha la Utamaduni

Na Eleuteri Mangi - WUSM, Dar es Salaam

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa ameipongeza Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa maandalizi mazuri waliyofanya ya kuan-daa Tamasha la kwanza la Kitaifa la Utamaduni ambalo haijawahi kufanyika tangu nchi ipate uhuru.

“Nafahamu yapo matamasha mengi ya Utamaduni hapa nchini ambayo yanaandaliwa na wadau mbalimbali, na machache yanaandaliwa na Serikali Kuu ama na Serikali za Mitaa. Kimsingi hii ni jitihada kubwa aliyoionesha Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhakikisha Utamaduni unakuwa kipaumbele katika nchi. Mheshimiwa Rais ana maono makubwa sana, anatutakia mema Watanzania” amesema Waziri Mkuu Majaliwa.

Kipekee ameshukuru uongozi wa Wizara wakiongozwa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Naibu Waziri Mhe. Pauline Gekul, Katibu Mkuu Dkt. Hassan Abbasi na Naibu Katibu Mkuu Ndg. Saidi Othman Yakubu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kusimamia vyema

Sekta ya Utamaduni.

Pia Waziri Mkuu ameshukuru na kupongeza Uongozi wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri kwa kufanikisha kufika kwa wadau kutoka nje ya Jiji la Dar es Salaam na kusisitiza kuwa anafahamu mikoani shughuli za Utamaduni hazipewi kipaumbele lakini kwenye hili wamefanya vizuri.

Aidha, amewashukuru washiriki wote kwa kuitikia wito wa kuja kwenye Tamasha hilo kuwa kuwa ni wadau muhimu katika kukuza, kuen-deleza na kuimarisha Sekta ya Utamaduni nchini.



Watu zaidi ya milioni kumi washuhudia Tanzania Utamaduni Carnival leo

Na John Mapepele – WUSM, Dar es Salaam

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mhe, Mohamed Mchengerwa amesema watu zaidi ya milioni kumi wameshuhudia matembezi ya kiutamaduni katika jiji la Dar es Salaam.

Mhe. Mchengerwa ameyasema haya wakati akimkaribisha Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano kwenye uzinduzi wa tamasha la kwanza la kitaifa la Utamaduni jijini Dar es Salaam ambapo amefafanua kuwa idadi hiyo inatokana na watu walioshiriki moja kwa moja na wale walioangalia kupitia vyombo mbalimbali vya habari.

Amesema kufanyika kwa tamasha hili la kwanza la kitai-

fa la utamaduni ambalo limejumisha matembezi ya kiutamaduni ni maono ya Mhe. Rais ya kutaka kukutani-sha utamaduni wetu.

Ameongeza kuwa upekee wa tamasha hili ni kuwa limeandaliwa mahususi kwenye maadhimisho ya kilele cha siku ya kiswahili duniani. Aidha, amefafanua kuwa Taifa lisilo na mila na desturi ni sawa na taifa lililo mateka na mufu.

Amemthibitishia, Mhe. Majaliwa, kuwa maelekezo aliyoyatoa kuhusiana na kuwa na mavazi ya taifa anakwenda kuyatekeleza mara moja. Amesema Machifu takribani 50 wameshiriki katika tamasha hili ambapo amesisitiza

kuwa Serikali itaendelea kuwaheshim na kuwatetea Viongozi hao wa kimila. Aidha amewashukuru machifu kujitua kwenye shughuli mbalimbali za Serikali hususan zoezi la kitaifa la sensa litakalifanyika Agosti 23, 2022.

Amesema tamasha hili ni la kipekee kwa kuwa limeshirikisha takribani mikoa yote ya Tanzania na limeshirikisha Utamaduni Carnival, usiku wa taarabu ambao utafanyika kwenye ufukwe wa Coco jijini Dar es Salaam Julai 3, 2022.

Ametoa wito kwa watu wengi kujitokeza kwa wingi kwenye usiku wa taarabu kwa kuwa hakuna kiingilio.



Matembezi ya Utamaduni Tanzania Yafana Jijini Dar es Salaam

Na Eleuteri Mangi - WUSM, Dar es Salaam

Siku njema huonekana asubuhi. Huu ni msemu wa Kiswahili na leo Julai 2, 2022 unasadifu ambapo Matembezi ya Kiutamaduni yamepamba moto kuzunguka mitaa ya jiji la Dar es salaam ambalo ni mwenyeji wa Tamasha la Kwanza la Utamaduni Kitaifa.

Mapema asubuhi kabla ya kuanza matembezi hayo, jiji la Dar es salaam lilipata baraka za rasharasha za mvua ambayo ni ishara njema katika Utama-

duni wa Mtanzania na Baraka ya Mwenyezi Mungu.

Hakika mitaa ya Kariakoo, Tandika, Mwembeyanga imetia fora kwa wananchi kujitokeza kwa wingi na kuwaunga mkono wanutamaduni kwa kucheza ngoma za makabila mbalimbali ya mikoa ya Mara, Pwani, Iringa, Njombe, Tabora, Mtwara, Kagera. Hakika siku ya Utamaduni imefana kwa kushangiliwa na

wananchi wa viunga vya jiji hilo.

Shamrashamra za Matembezi hayo ya Utamaduni zimeanzia Uwanja wa Benjamin Mkapa kuelekea daraja la Mfugale, daraja la Kijazi Ubungo, Morocco, Namanga, Coco Beach, daraja jipya la Tanzanite, Posta, Kariakoo, Stesheni, Mtoni kwa Azizi Ally, Temeke, Mwembeyanga na kurudi Uwanja wa Uhuru.



Vikundi vya Ngoma za Utamaduni Vyaisimamisha Dar

Na Shamimu Nyaki - WUSM, Dar es Salaam

Matembezi ya Kitamaduni yaliyofanyika mapema Julai 02, 2022 viunga vya Jiji la Dar es Salaam vimefanya jambo kubwa katika kuenzi Utamaduni wa Tanzania.

Akizungumza wakati akitoa salamu na neno fupi katika Uzinduzi wa Tamasha la

kwanza Kitaifa la Utamaduni, Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam, Naibu Katibu Mkuu Saidi Yakubu amesema katika maeneo Matembezi yalipopita Wananchi walijitokeza kwa wingi kushuhudia Utamaduni wa nchi yao.

"Tumekua na Vikundi kutoka

Mikoa takriban 24 ya Tanzania Bara na viwili kutoka Zanzibar, kwa hakika wana Dar es Salaam wameshuhudia Maonesho ya Mila na desturi za Taifa letu, Wameona, wamekumbuka na kutambua Utamaduni wa makabila yetu" amesema Bw.- Saidi Yakubu.



Mpoto apamba Tamasha la kitaifa la Utamaduni

Na John Mapepele, Dar es Salaam

Msanii maarufu wa muziki nchini Mrisho Mpoto amewawongoza wasanii kwenye uzinduzi wa Tamasha la kwanza la kitaifa la Utamaduni jijini Dar es Salaam

Uzinduzi huo umefanywa leo Julai 2, 2022. na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe, Kassim Majali-

wa.

Katika tukio hilo Mpoto alitumbuiza kwa wimbo wake mpya wa "titi la mama" wenye ujumbe mzito wa kuthamini Utamaduni ambao umekuwa kivutio kikubwa na kushangiliwa na wananchi hasa aliposisitiza kushiriki kikamilifu suala la sensa.

Aidha, kabla ya kuwasili kwa Mhe. Majaliwa wasanii mbalimbali wa kizazi kipya wametumbuiza.

Kaulimbiu ya tamasha hili ni Utamaduni wetu, fahari yetu, tushiriki kuhesabiwa. Kazi iendele.

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

**Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano
Serikalini - GEU**

Mawasiliano

P.O. Box 25, Dodoma, Tanzania
Mji wa Serikali Mtumba
Telephone: +255 26 2322 129
Nukushi: +255 26 2322 128
Barua pepe: km@habari.go.tz